# LBE Komputa na Intaneti – Programme 6

Mwandishi : Richard Lough, Kontanze von Kotze

Muhariri: Maja Dreyer

**Wahusika:** Beatrice (Msichana wa Makamu), John (Mvulana wa Makamu), , Sauti ya Komputa, Internet (Sauti )
Joe Kiki (Sauti ya Mwanamume), Joana (Mwanafunzi ), Salid (Mwanafunzi)
**Sauti Nyingine kutoka Studioni.**

**Package 6.1**

**Music – [Full up for 0.10 then fade under Intro]**

**Intro:**

Hujambao msikilizaji na karibu katikakipindi kingine kuhusu Komputa na Intaneti. Katika kipindi hiki , Beatrice na John wanataka kujua jinsi mtu anavyoweza kusoma kupitia mtandao wa Intaneti.. Si kila mtu anaweza kujiunga na shule au chuo kikuu, na hivyo mpango wa masomo kupitia mtandao wa Intaneti unaofahamika sana kama ***e-learning*** umeleta afueni kubwa kwa watu wengi vijana kwa wazee. Ungana nasi hadi mwisho wa kipindi ujifunze mengi kuhusu unavyoweza kutumia mtandao kupata elimu…...

**SFX Dialing_Up_Internet [Fade under…]**

**1.Komputa:** Habari John, Habari Beatrice…

**2. John:** Habari yako Komputa! Leo tunataka utufahamishe jinsi Mtu anavyoweza kutumia mtandao wa kupata elimu yaani ***e-learning***. Rafiki yetu ameshindwa kugharamia elimu ya chuo kikuu lakini ameambiwa anaweza kusomea digrii yake kupitia mtandao wa Intaneti. ….

**3. Komputa:** Hebu ngojeni kidogo nijiunganishe na mtandao…., mtandao unaelewa vizuri kuliko mimi. …

**3. Beatrice:** Asante sana Komputa

**4. Komputa:** Sasa tumeunganishwa. Habari Mtandao. Hapa tuko na rafiki wetu wawili, Beatrice na John, nadhani umekutana nao. Wangependa kujua zaidi kusumu masomo kupitia mtandao yaani ***e-learning.***

**5. Intaneti :** Habari Komputa, ni furaha yangu kuwasaidia. Kwa hivyo moja kwa moja tuanzie mpango huu wa mafunzo kupitia mtandao ***e-learning***… sivyo?

**6. Beatrice:** Ndio tafadhali Intaneti. Kwa kweli hatuelewi jinsi mtu anavyoweza kusoma na kufanya mtahiani wake kupitia mtandao wa Intaneti bila kuingia chuoni au shuleni.

**7. Internet:** Sawa, hivyo ndivyo nilivyorahisisha elimu na kuiweka wazi kwa ulimwengu. Sasa mtu yoyote anaweza kusomea mahali popote wakati wowote mradi tu ameunganishwa na mtandao wa Intaneti.

**8. John:** Na je waalimu ? Nani atakwaambia unachpasa kufanya,kukuelekeza na kazi za masomo nyumbani,kusahihisha kazi yako na kukupa gradi?

**9. Intaneti:** Kila ukurasa wa mfumo wa elimu kupitia Intaneti, una waalimu waliohitimu katika masomo yote ya kila aina, kama vile tu mwalimu wako wa kawaida shuleni au chuoni.. Tofauti ni kwamba wanafahamu vyema masuala ya Komputa na Teknolojia ya mawasiliano.

**10. Beatrice:** Inaonekana kazi ngumu na ya kuchokesha.!, Kusoma peke yako kupitia mtandao bila mwalimu wa kuzungumza naye au kukuelekeza.

**11. Intaneti :** Hapo ndipo watu wanapokosea, Beatrice. Ni kama vile tu mawasiliano ya moja kwa moja kupitia mtandao au hata kutumia kanda za video.

**12. Beatrice:** Kweli? Basi unaonekana ni mfumo mzuri. Sasa unaweza kutufungulia ukurasa huo?

**SFX_epals_site**

**13. Intaneti :** Sasa . Nadhani ukurasa huu utakuwa mfano mzuri. Unafahamika kama ***e-pals*** na hufanya kazi kama Darasa la jumuiya Ulimwenguni, ambapo unaweza kuwasiliana na wanafunzi wengine kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu..

**SFX Akiandika kwa komputa**

**14. Beatrice:** Ukurasa huu unasema ***"epals*** ni utanda wazi wa wasomi na waalimu kutoka zaidi ya mataifa 200 kote ulimwenguni.". Je hii inamaanisha naweza kujumuika na wanafunzi wengine kote ulimwenguni?

**15. Internet:** Ndio . Katika ukurasa huu kuna vifaa katika vinavyoweza kukutafsiria.Ukufungua sehemu iliyoandikwa ***Projects*** na uende kwa orodha ya yaliyomo yaani ***menu*** utakuta maada mbali mbali ambazo zinaendelea kujadiliwa na wanafunzi na waalimu .

**16. John:** Utaweza kuona masuala kuhusu mabadiliko ya hali ya anga, ramani na mikasa mbali mbali ya kimaumbile inayotokea duniani.

**17. Beatrice:** Kisha unaweza kujumuika au kushiriki mijadala hii kupitia mawasiliano ya moja kwa moja katika Intaneti.

**18. Intaneti :** Ukurasa mwengine unaoweza kujifunza masomo ya hesabu na ujuzi wa aina mbali mbali ni ule unaofahamika kama ***GCFlearnfree.org.***

**SFX_akiandika kwenye komputa.**

**19.Beatrice:** Sawa sasa naufungua ukurasa..

**SFX_akiandika**

**20. Beatrice:** Wewe, sio Hesabu tu!. Hata mafunzo ya ujuzi mbali mbali pia yana manufaa makubwa maishani

Kwa mfano kutuma maombi ya kutafuta kazi na kuoka.

**21. John:** Nimefurahishwa sana na mfumo huu wa elimu kupitia mtandao wa ***e-learning***. Ni tofauti kabisa na mifumo tunayozingatia hasa barani Africa. Hiki ndicho kinacho nifurahisha zaidi kuhusu mtandao wa Intaneti, unajifunza mambo mengi tena haraka sana .

**22. Internet:** Kabukeni John Beatrice, pia kuna kurasa nyingi zenye mifumo hii ya ***e-learning*** . Mukitaka kurasa nyingine munaweza kwenda kwa ukurasa wa ***Google***. Lakini ni lazime muhakikishe kuwa kurasa hizo zimeidhinishwa. Kwani ni lazima uwe waangalifu munapotumia huduma za Intaneti. Natumai tutaweza kukutana tena..

**23. John & Beatrice:** Asante Intaneti..

**Muziki (fade under…)**

**SFX Wanafunzi wanaingia darasani na kufungua mikoba yao ya vitabu**

**1. Beatrice:** Niko katika darasa la mafunzo ya Komputa katika shule ya sekondari ya Agnes Miegel iliyoko mji mkubwa wa Düsseldorf, Magharibi mwa Ujerumani. Niko hapa kujifahamisha jinsi wanafunzi wa shule hii wanavyo wasiliana moja kwa moja na wenzao nchini Togo Magharibi mwa Africa, kupitia mtandao wa Intaneti. Kila siku ya Jumanne kundi la wanafunzi 20 hukutana hapa kuwasiliana na wenzao nchini Togo kupiti mtandao wa Intaneti.

**SFX: Komputa ikifunguliwa**

**2. Beatrice:** Mradi huu unasimamiwa na Mwalimu kwa ushirikiano na Joe Kiki raia wa Togo ambaye amekuwa akiishi nchini Ujerumani kwa miaka kadha sasa. Wanafunzi wengi hufurahia mawasiliano ya moja kwa moja na wanafunzi wengine wanapounganishwa kupitia mtandano na idadi hiyo inazidi kuongezeka kila mara.

**Clip: 6.2_Kiki_1 ( Kifaransa)**

“ Hapa ni kana kwamba kunasherehe fulani, maana kila siku unajifunza mambo mapya na mazuri kama ambaye

uko mbinguni. Ni furaha iliyoje kuzungumza na watu walioko umbali wa zaidi ya kilomita 7000. Mimi naelewa jinsi mtandao unavyofanya kazi, Ni jambo linalonifurahisha zaidi licha ya kwamba nimekuwa nikitumia huduma hizi.".

**3. Beatrice:** Kwa kweli, huduma hizi za mawasiliano ya mtandao ni kama aina nyingine yoyote tu ya mawasiliano .Kwa upande mmoja unakuwezesha kubadilishana habari kwa haraka na kisha unaweza kumuona mwenzako upande mwengine, hii yote imewezekna kupitia kamera iliyoko kwenye mtandao. Na hii ndiyo tofauti kubwa kati ya barua pepe na huduma hizi za mawasiliano ya papo hapo.

**SFX: Wakizungumza**

**4. Beatrice:** Hivi sasa, Joana anamuandikia rafiki yake nchini Togo. Hebu nimuulize huduma hizi zinavyofanya kazi.

**Clip: 6.2_Joana_1 (German)**

" Huyo ni rafiki yangu kutoka Togo. Ananieleza kuwa walikuwa na ugonvi na mpenzi wake wa kiume. Habari hiyo imenigusa sana ni kama ambayi ni mimi, na ningetaka kujua zaidi jinsi walivyosulughisha mzozo huo"

. **(SFX akiandika kwenye komputa**.)

"Namuuliza walivyotatua mzozo huo. Na sasa nasubiri anijibu- Ahha, ameandika kusema kuwa mpenzi wake anataka kusomea taaluma ya utendaji na yeye hajafurahia jambo hilo.."

**(SFX akiandika tena)**

**Beatrice:** Ahha ni ajabu sana, kumbe ni rahisi, yaani Joanna anandika na rafiki yake anamjibu papo hapo licha ya kwamba wako umbali wa maelfu ya kilomita .Mbali na hayo wanaweza kuzungumza naye ana kwa ana . Sawa, hapa pia kuna Salid, hebu tuone anafanya nini.

**Clip: 6.2_Salid_1 (German)**

" Huyu ni rafiki yangu niliyemjua kupitia Joana na sasa tumekuwa tukiwasiliana mara kwa mara Anasema kuwa anafuraha kwa kuwa amerejea shuleni baada ya Kupata pesa. Alikuwa amekatiza masomo kutokana na ukosefu wa karo.

**(SFX akiandika )**

**Beatrice:** Na mawasiliano yote haya wanafanya katika muda wa sekunde kadhaa tu. Huduma hizi za Intaneti hufanya mambo kuwa rahisi sana anasema Joana.

**Clip: 6.2_Joana_2 (German)**

" Mawasiliano haya ni kama ufariki tu. Munnaweza kuzungumza mambo ya shuleni na waalimu, pia mambo yenu ya siri wakati wote mtakao."

**Beatrice:** Vijana wengi nchini Ujerumani na Togo wanatafakari za aina moja na kufanya mambo yaliyo sawa.

**Clip: 6.2_Salid_2 (German)**

" Ndio ni furaha kubwa kuwaelimisha jinsi tunavyoishi hapa Ujerumani na wao pia kutuelezea maisha yalivyo nchini Togo.."

**Beatrice:** Kwa raia huyu wa Togo Joe Kiki, kufahamikiana ndio msingi zaidi wa mradi huu wa ushirikiano baina ya shule.

**Clip: 6.2_Kiki_2 (French)**

"Hilo ndilo lengo kubwa la muda mrefu. Utawezaje kufahamikiana na watu kutoka pembe nyingine za ulimwengu? Njia pekee ya kuwasiliana na kupitia mtandao huu wa Intaneti. Kwa hivyo ni lazima tufanye kila tuwezalo kukuza na kuzipa umuhimu huduma hii. Teknolojia inabadilika kwa haraka na watoto wetu pia ni sharti wabadilike kulinga na mabadiliko hayo ulimwenguni."

**Beatrice:** Joe anasema kuwa changamoto kubwa ni kuwahamasisha wazazi nchini Togo kuhusu teknolojia hii. Wazazi hawa wanaamini kuwa huduma hizi pamoja na kawi ni ghali mno. Kadhalika wanaamini kuwa huduma hizi za mawasiliano zinatatiza na si muhimu kwao.

**Clip: 6.2_Kiki_3**

"Unaweza kufikiri kwamba ni vigumu lakini punde unapojitosa katika ulimwengu huu, kila kitu huwa rahisi. Na manufaa yake? Kwa kweli unaweza kutumia mtandao kurekebisha dhana mbaya miongoni mwa watu. Kwa mfano raia wa Togo wanaamini kuwa Ujerumani ni kama peponi huku watu wengi wakilitizama bara la Africa kama bara linalogubikwa na Umaskini"

**Muziki**

**Outro:**

Na ni hayo tu kwa leo ambapo tumejifunza vipi komputya na mtandao wa Intaneti zinavyotumika kuelimisha umma na kujenga ushirikiano wa kimasomo ulimwenguni. Katika kipindi kijacho tutajifunza zaidi kuhusu matumizi ya kanda za Video na sauti kwenye Intaneti. Kumbuka ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki unaweza kutembelea tovuti yetu: www.dw-world.de . Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa.!

***Mwisho***